

MPANGO WA USAJILI NA KUTOA VYETI VYA KUZALIWA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA MITANO WAZINDULIWA MKOANI IRINGA

HABARI NA PICHA ZA MATUKIO



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe Dkt Harrison Mwakyembe akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Mpango wa Kitaifa wa Usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa Watoto wenye Umri chini ya Miaka mitano kwa Mkoa wa Njombe na Iringa. Uzinduzi ulifanyika katika Viwanja vya Mwembetogwa Mkoani Iringa. Wengine kutoka kushoto ni Mwakilishi Mkazi wa UNICEF Bi Maniza Zaman, Mkuu wa Mkoa wa Iringa Mhe. Amina Masenza, Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Dr. Rehe-ma Nchimbi na Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya RITA Prof Hamisi Dihenga.

'Mtoto anastahili Cheti cha Kuzaliwa, mpe Haki yake'

PICHA NA MATUKIO



Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria, Mhe. Dkt Harrison Mwakyembe akikabidhi Cheti cha kuzaliwa kwa Mama wa Mtoto wa kwanza kusajiliwa katika Mpango wa Usajili na Kutoa Vyeti vya Kuzaliwa kwa Watoto wa Umri chini ya Miaka Mitano .



Mhe Waziri Dkt Harrison Mwakyembe akifurahia jambo na moja ya mtoto aliyesajiliwa na kupata cheti cha Kuzaliwa Mkoani Iringa.



Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria, Mhe. Dkt Harrison Mwakymbe akiwa katika picha ya Kumbukumbu na Viongozi wa Mikoa wa Iringa na Njombe pamoja na sehemu ya Wazazi na Watoto waliosajiliwa na kupata Vyeti vya Kuzaliwa.



Sehemu ya Burudani katika Uzinduzi wa Mpango wa Usajili na kutoa Vyeti vya Kuzaliwa kwa Watoto wa Umri chini ya Miaka Mitano Katika Mikoa wa Iringa na Njombe